Toleo 88 - Shawwal 1445 H / Mei 2024 M

# UQAB

Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Imarati (UAE) Yaunda Kikosi cha Mamluki, ambacho Baadhi yake Kitafanya kazi nchini Yemen na Sudan!

**HABARI NA MAONI**
Kinyang'anyiro cha Uagizwaji wa Pombe ni Kielelezo cha Maangamizi ya Utalii Zanzibar

**MATOLEO**
Kisha Nini Kinachofuata, Enyi Waislamu?

**JIBU LA SWALI**
Hadith
«إِنَّ الإِسْلامَ يَجُبُّ مَا كَانَ قَبْلَهُ»
"Hakika Uislamu Hufuta Yale Yalikuwa Kabla Yake"



## Mtazamo wa Haraka kuhusu Kifo cha Jenerali Ogolla

Afisi ya Habari Kenya

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 13/1445 Jumanne, 14 Shawwal 1445 H 23/04/2024 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Mtazamo wa Haraka kuhusu Kifo cha Jenerali Ogolla

Hatimaye Jenerali Francis Ogolla amezikwa. Baada ya kifo na mazishi, kuna haja ya kuzingatia mambo yafuatayo:

Kifo ni janga na somo. Janga kwa maana kwamba watu wenye hadhi ya juu wanapofikwa na kifo cha ghafla hupelekea dukuduku na wasiwasi ambapo wanasiasa hutumia fursa hii katika kufikia malengo yao ya kisiasa hivyo kusababisha hali ya vurugu au maridhiano. Hakika pia ni somo kwa wote, bila kujali wadhifa wako, cheo, hadhi na tabaka kifo ni uhalisia usioepukika.

Kwa kuwa tunaishi katika jamii ya kiliberali-kisekula, kifo huonekana chenyewe kuwa kikomo. Usekula hunamlazimisha mwanadamu kutenganisha maisha ya kidunia na kifo na hivyo kumsukuma kuzama katika ulimwengu wa kimada kama njia pekee ya kutoroka. Kinyume chake, Uislamu unakiona kifo kuwa sio kikomo ndani yake bali kuna maisha baada ya kifo, kwamba tutahesabiwa kwa kila kitendo tulichofanya na tutapelekwa Jannah (Peponi) au Jahannam (Moto wa Jahannam) kulingana na matendo yetu.

Bila kujali maoni tofauti kuhusu kifo cha Jenerali Ogolla, ni muhimu kuweka wazi kuwa kuna ombwe la uaminifu na mpasuko katika uongozi wa kidemokrasia. Demokrasia kimsingi inawanyima tabaka la kisiasa kuaminiwa, haki na uhuru kutokana na ushawishi wa kikoloni na waungaji mkono. Kwa hivyo kifo cha Jenerali Ogolla na kama ilivyo kwa viongozi wengine wa ngazi za juu kitabaki kuwa na dukuduku.

Kwa vile siasa ni sehemu muhimu ya maisha, Uislamu umefasili siasa kuwa ni kitendo cha ibada inayomdhamini yeyote anayeshika nafasi ya kisiasa kubeba jukumu kubwa mbele ya Allah (swt). Kwa hivyo wakati wowote kifo kama hicho kikitokea hakitaanikwa kwa uvumi ambao unaweza kusababisha kukosekana kwa utulivu lakini badala yake kuvipa vyombo vyote vya dola kutoa taarifa wazi juu ya suala hilo.

Uteuzi wa haraka na upesi wa kaimu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi (CDF) umeonyesha wazi umuhimu mkubwa wa uongozi katika jamii yoyote ile. Ni bahati mbaya sana kwa Umma wa Kiislamu kwa miaka mia moja leo bila kiongozi! Haishangazi Waislamu wako hatarini kwa kila aina ya udhalilishwaji, ukandamizwaji, dhulma na mauaji ndani ya nchi za Kiislamu na duniani kote. Mfano hai ukiwa Gaza leo ambapo IDF ya umbile la Kiyahudi inafanya mauaji ya halaiki bila kuadhibiwa. Kwa udharura wake, Umma wa Kiislamu unawajibika kufanya kazi kusimamisha tena chombo cha kisiasa (Khilafah) ambacho kitahakikisha usalama na uadilifu kwa wanadamu wote.

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

**Afisi ya Habari Wilayah Yemen**

حزب التحرير

HIZB UT TAHRIR

KUMB: 30/1445 Jumapili, 12 Shawwal 1445 H 21/04/2024 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Imarati (UAE) Yaunda Kikosi cha Mamluki, ambacho Baadhi yake Kitafanya kazi nchini Yemen na Sudan!

Uchunguzi uliochapishwa na gazeti la Ujerumani Deutsche Welle mnamo tarehe 14/04/2024 uliisifia UAE kama kituo cha mamluki barani Afrika na Mashariki ya Kati, haswa Yemen na Sudan. Gazeti la Ufaransa, Online Intelligence lilifichua tangazo hilo, ambalo lilisambazwa kwa wanajeshi wa zamani katika Kikosi Maalum cha Ufaransa. Gazeti hilo lilieleza kuwa uchunguzi ulionyesha kuwa tangazo hilo ni la Kampuni ya Ushauri wa Kijeshi ya Manar, ambayo inaendeshwa na afisa wa zamani wa Kikosi Maalumu cha Ufaransa chenye uhusiano na Abu Dhabi. Jarida la Ufaransa lilisema kwamba mtu anaweza kuhitimisha kutokana na tangazo hilo kwamba UAE inataka kuunda vikosi vyake vya bora vya kigeni, labda vinavyojumuisha idadi ya wanajeshi kati ya 3,000 na 4,000, kufikia katikati ya 2025. Jaribio la kwanza la Abu Dhabi lilikuwa mwaka 2009 kuunda brigedi ndani ya Imarati yenye wanachama 800 na Erik Prince, mwanzilishi wa Blackwater.

Imarati, mtoto wa Waingereza, ambayo idadi ya jeshi lake ni 65,000, ilianza kutumia mamluki wa kigeni mwaka 2016 ilipokodi mamluki kutoka kampuni ya American Spear Group kuwaua watu 160 ambao hawakutii amri yake, wakiwemo maimamu, wahubiri wa misikiti, wanasiasa, wanajeshi, na wanasheria wa Aden, baada ya UAE kuingia nchini humo kuwafukuza Mahouthi mnamo Agosti 2015. Ushirikiano uliendelea kati ya maafisa wa Marekani na maafisa wa Imarati, kama shirika la Reuters lilivyofichua mwaka wa 2019 kwamba UAE ilikuwa inataka kuanzisha vitengo vya vita vya kielektroniki. Gazeti la Washington Post pia liliripoti mwaka 2022 kwamba UAE inaendelea kulipa mishahara kwa maafisa wa zamani wa kijeshi wa Marekani badala ya kutoa huduma na ushauri. Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Amani ya Stockholm, Sipri, mwaka 2023, hali ya makampuni ya ulinzi ya kijeshi ya kibinafsi imeongezeka tangu 2003, tangu kuanzishwa kwa Blackwater na dori yake chafu katika uvamizi wa Iraq.

Leo, Abu Dhabi inaonekana katika hali mbaya zaidi, inapoanzisha kikosi cha mamluki kuhudumia miradi ya kikoloni ya Uingereza nchini Yemen na Sudan. Ama kwa Yemen, kutekeleza mauaji zaidi yaliyoanza mwaka 2016 ili kuunga mkono mipango ya Uingereza, kukabiliana na kuzuia mipango ya Marekani. Na nchini Sudan kusaidia nguvu za uhuru na mabadiliko ambazo zilizibwa pumzi na mizozo ya jeshi la Marekani; Al-Burhan na Hamidati; vilevile Somalia, Libya na kwingineko.

UAE inafanya hivi ili kumtumikia bwana wake, Uingereza, na kuwa sambamba na mipango ya Marekani katika Mashariki ya Kati. Inadaiwa na Waingereza uaminifu kamili na utiifu, kama mataifa yote mengine ya Ghuba, isipokuwa Saudi Arabia, ambayo inafuata utawala wa Marekani wakati wa enzi ya Salman na mwanawe ... Kwa hivyo, kugongana dhahiri katika sera yake ni matokeo ya mistari mipana iliyochorwa na Uingereza kwa ajili yake kwa kuungwa mkono na watu masekula na wanamgambo wa Kiislamu wanaopinga. Aidha, UAE inatekeleza sera maalum na za kina za Uingereza, na hiyo, UAE, mara nyingi huifanyia kazi Uingereza kwa safu ya nyuma ya vibaraka wa Marekani katika kanda hii, na hutoa huduma zake kwa Uingereza kutoka maeneo hayo.

Hivi ndivyo serikali tawala katika nchi za Kiislamu zinavyonyauka na kuoza baada ya kujiondoa katika utawala wa Uislamu na kuubeba kwa wasiokuwa Waislamu, na kujihusisha na mipango ya maadui wa Uislamu na Waislamu, kama vile Imarati ambayo imekuwa kimbilio la wasiokuwa Waislamu ambao idadi yao inazidi idadi ya watu wao, na wanajenga makanisa, masinagogi na mahekalu ya Kibaniani ya ushirikina kwa ajili yao, na kuanzisha majeshi ya kutumikia ukafiri na watu wake, na dhidi ya Uislamu na watu wake katika Bara Arabu! Mwenyezi Mungu (swt) asema:

الأَعْرَابُ أَشَدُّ كُفْراً وَنِفَاقاً وَأَجْدَرُ أَلاَّ يَعْلَمُواْ حُدُودَ مَا أَنزَلَ اللهُ عَلَى رَسُولِهِ وَاللهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ * وَمِنْ الأَعْرَابِ مَنْ يَتَّخِذُ مَا يُنفِقُ مَغْرَماً وَيَتَرَبَّصُ بِكُمُ الدَّوَائِرَ عَلَيْهِمْ دَائِرَةُ السَّوْءِ وَاللهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

"Na katika Mabedui hao wapo wanao fikiri kuwa wanayo yatoa ni gharama ya bure, na wanakungojeleeni mambo yakugeukieni. Mageuko maovu yatakuwa juu yao! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua." [At-Tawbah 9:98]. Kazi na matarajio ya Waislamu itanasilia katika kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume ambayo Hizb ut Tahrir inaifanyia kazi na kuilingania kwa Waislamu ili kuitikia ulinganizi huu mtukufu wa kufikia haki na kuifagia mipango miovu dhidi ya Uislamu na Waislamu.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Yemen**

# Kisha Nini Kinachofuata, Enyi Waislamu? Je! Mnasubiri nini baada ya kushuhudia kile kilichotokea huko Gaza? Je! Sio wakati wa nyinyi kusonga na kuitikia amri ya Mola wenu Mlezi kwa kusimamisha Khilafah Rashida?



Siku chache tu zilizopita, kumbukumbu ya kuvunjwa Dola ya Kiislamu baada ya miaka 103, katika mwezi wa Rajab Tukufu, sanjari na maadhimisho ya Al-Isra Wal Mi'raaj mwezi huo huo. Mwenyezi Mungu (swt) amesema:

[سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلاً مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الأَقْصَى الَّذِي
بَارَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنْ آيَاتِنَا إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ البَصِيرُ]

**"SUBHANA, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona."** [Surat Al-Isra:1].

Mwenyezi Mungu (swt) amenasibisha kati ya Masjid Al-Haram na Masjid Al-Aqsa katika uhusiano wa kiitikadi, wa milele katika Quran yake hadi Siku ya Kiyama. Walakini, inaomboleza na inaita mchana na usiku kwa ajili ya ukombozi wake kutoka kwa uvamizi wa umbile la Kiyahudi, mbele ya macho na masikio ya watawala wa Ruwaibidha (watepetevu) wa makasri, lakini hakuna wa kujibu.

Na maadhimisho haya yanapita, na mito ya damu inayotiririka kutoka kwa watoto wa Waislamu huko Gaza, na udhalimu na ukatili wa umbile ovu la Kiyahudi umeenea kwa wanadamu, mawe, na miti kwa msaada wa ukoloni wa Marekani na Ulaya na usaliti wa watawala wa Kiarabu na nchi za Waislamu. Hakuna mtu muongofu katika majeshi ya Waislamu anayeongoza majeshi ya Waislamu kuunusuru Uislamu na Waislamu kwa kuliangamiza umbile la Kiyahudi huko Palestina na kuirudisha yote katika ardhi za Uislamu.

Kwa zaidi ya karne moja, Ummah wa Kiislamu umekuwa ukikabiliwa na kipindi kibaya zaidi katika historia. Kuvunjwa kwa Khilafah kulikuwa matokeo ya juhudi chafu, miongo kadhaa ya kupanga njama, na khiyana kutoka kwa dola za kikoloni za Magharibi katika mapambano yao dhidi ya hadhara ya Kiislamu hadi leo. Kuvunjwa kwa Khilafah hakukuwa matokeo ya adha ya kisiasa inayofanywa na dola za kikoloni za Magharibi, lakini badala yake matokeo ya juhudi, njama, na khiyana kutoka kwa dola hizo. Ilikuwa ni jambo la kimaumbile kwa dola hizi za kikoloni za Kikafiri kuhifadhi mafanikio yao kwa kujitahidi kuzuia kurudi kwa Khilafah, ambayo walikuwa wameshaivunja.

Uhalisia ambao Ummah inakabiliwa nao leo, haswa baada ya Vita vya Gaza, unaonyesha kwamba Ummah wa Kiislamu sasa unazidi kuitazamia Khilafah, umoja wa Kiislamu, na utabikishaji wa Sharia katika nyanja zote za maisha. Utambuzi na kushikamana kwa Ummah kwa Uislamu leo ni makubwa zaidi kuliko hapo awali, na Ummah sasa amejiandaa kikamilifu kutoa muhanga mmoja baada ya mwingine kwa sababu ya Dini yake. Hili

***Endelea... UK 5***

linasukumwa na fahamu zilizowekwa za aqeedah (itikadi) ndani yake na utambuzi wake wa kihisia kwamba hakuna wokovu kwake katika hali yake ya sasa isipokuwa kupitia kurudi Uislamu kupitia kusimamisha dola yake.

**Hapa, ni muhimu kufafanua ukweli ufuatao:**

1- Kwamba sisi ni Waislamu walioumbwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, na Uislamu umetuonyesha jinsi ya kuunda dola yenye nguvu, ikifafanua malengo yake ya juu ambayo yanastahiki heshima ya binadamu, ambayo inaweza kupatikana tu na dola inayotabikisha amri za Mola wa Walimwengu.

2- Hakika, Uislamu ndio dini ambayo Mwenyezi Mungu ameichagua kwa wanadamu, kwa hivyo hairuhusiwi kukubali itikadi zengine au mifumo yoyote iliyotungwa na mwanadamu. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

**[وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِيناً فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ]**

**"Na anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye kukhasiri."** [Surat Aal-i-Imran:85].

3- Khilafah ndio wajibu mkubwa ambayo kwayo faradhi kuu tatu zinapatikana: kusimamisha Dini, kuwaunganisha Waislamu, na kueneza Uislamu kote ulimwenguni. Ummah hauwezi kutimiza Uislamu na kuueneza isipokuwa wanapokusanyika chini ya mtu mmoja anayesimamisha Dini. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema:

**«مَنْ خَلَعَ يَداً مِنْ طَاعَةٍ، لَقِيَ اللهَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ لَا حُجَّةَ لَهُ، وَمَنْ مَاتَ وَلَيْسَ فِي عُنُقِهِ بَيْعَةٌ، مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّةً»**

**"Yeyote mwenye kuondoa mkono wake kutoka katika utiifu (kwa Amiri) atakutana na Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama akiwa hana hoja na yeye; na yeyote anayekufa na hana katika shingo yake ahadi ya utiifu (Bay'ah) amekufa kifo cha Kijahiliya."**

4- Dola za Kikafiri za Magharibi ni maadui wa Uislamu na watu wake. Uhusiano nazo lazima uwe ule wa kivita; Hazipaswi kuchukuliwa kama marafiki au washirika, na hazipaswi kuruhusiwa kuwa na uwepo au kambi za kijeshi nchini. Dola hizi, zikiongozwa na Marekani na Uingereza, hazisazi juhudi yoyote katika kuwauwa Waislamu, kupora utajiri wao, na kupanda mbegu ya mgawanyiko kati yao. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

**[وَلَن يَجْعَلَ اللهُ لِلْكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلاً]**

**"wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini."** [Surat An-Nisa:141].

5- Watawala wa nchi za Kiarabu na ardhi za Waislamu ni vibaraka wa Kafiri mkoloni na wafuasi wake. Ni maadui wa Ummah na Dini yake, na ndio kichwa cha Kafiri katika nchi za Waislamu. Hawasazi juhudi yoyote kuupiga vita Uislamu, kueneza ufisadi na uzinzi, kuuweka mateka Ummah wa maadui wa Uislamu, na kupuuza nusra yao kwa watu wa Gaza, ambayo iko dhahiri.

6- Asasi za kimataifa katika aina zao zote, kama vile Umoja wa Mataifa, Baraza la Usalama, Mahakama ya Haki ya Kimataifa, UNRWA, na nyenginezo, na pia taasisi za kikanda kama vile Ligi ya Kiarabu, Baraza la Ushirikiano la Ghuba, na Shirika la Ushirikiano wa Kiislamu, ni zana za dola za wakoloni wa Magharibi kudumisha utawala wao na kutekeleza mipango yao ya kupambana na Uislamu na kudumisha kutengana kwa Ummah wa Uislam na kunyimwa rasilimali zake.

7- Ukombozi wa Ummah kutokana na ukoloni unaweza kupatikana tu na vikosi halisi vya Ummah kusonga kuwapindua watawala madhalimu na kung'oa ushawishi wa ukoloni kutoka mizizi yake. Hili linahitaji kuunganishwa kwa vikosi vya Ummah ili majeshi ya Ummah yalingane na Uislamu na kujiunga na safu za Ummah, kutangaza kujitega kwao kutoka kwa serikali hizi za vibaraka, na kuharakisha kuzipindua na kuuacha huru Ummah kutokana na maovu yao.

Vita vya Gaza bila shaka vimethibitisha kwamba Ummah wa Kiislamu ni Ummah wa Jihad na Shahada, kupitia uthabiti wa watu wake na shujaa wake Mujadina ambaye alitikisa umbile oga la wanyakuzi wa Kiyahudi, licha ya idadi yao ndogo, rasilimali haba, na njama ya watawala. Kwa hivyo, tunawathibitishia Waislamu na wale ambao wana nguvu kati yao kwamba gharafa ya kafara watakayotoa kwa ajili ya kusimamisha Khilafah ni chini sana kuliko ile wanayolipa hivi sasa kwa sababu ya kukosekana Khilafah yao.

**Enyi Waislamu, Watu wa Nguvu na Azma nchini Jordan:**

Kadhia ya kufanya kazi kwa ajili ya kurudi kwa Khilafah ni kadhia nyeti ya Ummah, ambayo kwayo mtu lazima awe tayari kuchukua maamuzi ya uhai na kifo. Jaribio la dhati na kubwa, pamoja na wafanyikazi wanaofanya kazi mchana na usiku, linahitajika kuleta kurudi kwake kama nguvu kubwa ambayo huhifadhi nchi, watu wake, na utajiri wao. Kazi ya kivitendo kuelekea usimamishaji wake inahitajika kwamba watu wa nguvu na azma warudishe mamlaka kwa Waislamu na kuondoa mtu yeyote anayesimama kwa njia yao, iwe ni watawala, duara za ndani za ufisadi, au wasomi wenye madhara, na nyuma yao, msukumo wa ukoloni wa Magharibi. Tunaona kupatikana kwake kuwa karibu, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu; Ni ahadi ya Mwenyezi Mungu (swt), na bishara njema ya mjumbe wake (saw). Ummah mzima unatarajia siku ambayo dola yao itaregeshwa, kuwaokoa watu wa Palestina, Gaza, Al-Aqsa, na Waislamu wote wanaokandamizwa duniani.

# HABARI NA MAONI
# Kinyang'anyiro cha Uagizwaji wa Pombe ni Kielelezo cha Maangamizi ya Utalii Zanzibar

**Habari:**

Mnamo tarehe 04 Aprili 2024 Mahakama Kuu ya Zanzibar ilitupilia mbali Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kudhibiti Vileo (LCA), ikikiita kifungu hicho ni kinyume cha Katiba. Sheria hiyo iliyopitishwa mwaka 2020, ilipunguza idadi ya kampuni zinazoruhusiwa kuagiza pombe kutoka nje. Kifungu hicho kilidhibiti vibali vya kuingiza vileo viwe kwa ajili ya makampuni yanayomilikiwa na Wazanzibari na kuweka idadi jumla ya makampuni hayo iwe matatu tu.

**Maoni:**

Uamuzi huu wa mahakama ulikuja kufuatia shauri lililowasilishwa mahakamani na kampuni ya QMB kwamba waliagiza bidhaa ili kuepusha usumbufu kabla ya kibali chao cha awali kumaliza muda, na ombi lao la kukihuisha kibali hicho lilikataliwa. Uamuzi huu wa mahakama ulitengua uamuzi wa Bodi ya Kudhibiti Vileo Zanzibar (ZLCB) wa kutoa leseni kwa makampuni matatu mapya ya kuingiza vileo ambayo ni: Kifaru, Bevko na Zanzi Imports na kuchelewesha kuhuisha vibali kwa waagizaji watatu wa awali- QMB One Stop, Scotch Store na ZMMI.

Lazima ieleweke bayana kwamba uamuzi wa bodi wa kudhibiti waagizaji wa pombe haukutokana na sababu za kulinda maadili au maslahi yoyote ya Ummah, lakini huenda ulitokana na rushwa na ushiriki wa baadhi ya vigogo katika makampuni mapya yaliyopewa vibali kuagiza pombe. Uamuzi huo wa Mahakama unaongeza ushindani katika soko la pombe na uingizaji wake Zanzibar. Unailazimisha Bodi ya Kudhibiti Vileo Zanzibar (ZLCB) kuyapa makampuni mengi zaidi haki ya kuagiza pombe kutoka nje ya nchi. Tukio hili ni dhahiri kuwa inaonyesha taswira ya kusikitisha ya kuzorota kwa maadili na silka njema ndani ya Zanzibar.

Uislamu umekuwa sehemu ya utamaduni wa Zanzibar tangu watu wa visiwa hivi walipoukubali Uislamu kati ya karne ya 7 na 8 Miladi, huku Zanzibar ikiwa na wakaazi Waislamu 99.9%.

Hivyo, ni zaidi ya aibu ya kiwango cha juu kwa serikali ambayo asilimia 99.9 ya wakaazi wake ni Waislamu kujizatiti katika kueneza ulevi unaopelekea uharibifu kwa utamaduni wa Kiislamu ndani ya Zanzibar kwa ajili ya maslahi binafsi tu na kuuvutia utamaduni wa kikoloni wa Kimagharibi kwa jina la utalii.

Zanzibar kama zilivyo biladi nyingine nyingi za Waislamu imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi ikiwemo gesi asilia, kuzungukwa na Bahari ya Hindi nk. lakini imelazimishwa kutegemea sekta ya utalii kama chanzo chake kikuu cha mapato, na umekuwa utalii unachangia asilimia 90 ya mapato ya nje ya visiwa hivyo.

Utalii umekuwa chanzo kikubwa cha mporomoko wa maadili ndani ya Zanzibar, watalii kutoka nchi za Magharibi wamekuwa wakiingiza visiwani humo uchafu na maadili maovu yatokanayo na mfumo wa kibepari kama vile ulevi, matumizi ya dawa za kulevya, ushoga, uasherati, mavazi yasiyo ya staha nk. Kwa kweli utalii umeporomosha maadili ya Kiislamu ya Zanzibar na umekuwa chanzo cha maafa katika ardhi zetu.

Uamuzi wa mahakama unatilia mkazo ukweli wa mtazamo wa kidemokrasia katika nyanja mbili: Kwanza, maadili ya kisekula ni yenye kupuuza mwongozo wa kiungu na badala yake huipa akili dhaifu ya mwanadamu nguvu za kusimamia mambo ya wanadamu.

Pili, serikali za kisekula hazijali ustawi wa watu wao, kutokana na ukweli kwamba pombe inachangia zaidi ya 21.7% ya ajali za barabarani nchini Tanzania, lakini badala ya kufanya juhudi kubwa za kukomesha, uingizaji wake ndio unahamasishwa na kuimarishwa.

Uislamu una suluhisho adhimu na madhubuti kwa kila tatizo la mwanadamu ikiwemo ulevi. Suluhisho la Kiislamu kwa jambo hilo ni rahisi, la kivitendo na la busara. Uislamu unakataza ulevi kwa namna yoyote ile, Mwenyezi Mungu (swt) anasema katika Quran Tukufu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالأَنصَابُ وَالأَزْلاَمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ

**"Enyi mlioamini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya shet'ani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa."** [Al Maidah 5: 90]


Kupitia katazo hili, dini, mali, utu na jamii kwa ujumla italindwa kwa ajili ya maslahi mapana ya ustawi wa binadamu.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Said Bitomwa**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

**JIBU LA SWALI**

# Hadith «إِنَّ الإِسْلاَمَ يَجُبُّ مَا كَانَ قَبْلَهُ» "Hakika Uislamu Hufuta Yale Yalikuwa Kabla Yake"



**Swali:**

Assalam Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Ndugu Mpendwa, salamu njema kwako,

Katika kitabu, Kielelezo cha Katiba, Juzuu I, Kifungu 95

cha eleza yafuatayo:

(Ama kushughulika na kesi zinazodhuru Uislamu na Waislamu, hii ni kwa sababu Mtume aliamuru kuuawa kwa watu wachache waliosababisha madhara kwa Uislamu na Waislamu katika zama za Jahiliyyah baada ya ufunguzi wa Makka, na hivyo waliuawa hata kama walijifunga kwenye mapazia ya Al-Kaaba, kwa kujua kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema, إن الإسلام يجب ما قبله **"Hakika Uislamu Hufuta Yale Yalikuwa Kabla Yake"** (imepokewa na Ahmad na Al-Tabarani kutoka kwa Amr b. Al-As); kwa maneno mengine, yeyote anayeudhuru Uislamu na Waislamu haingii katika riwaya hii)

Nimechunguza uhalisia wa watu hawa na nikagundua kuwa baadhi yao walikuwa Waislamu na wakaritadi na wengine hawakusilimu na waliuawa. Kwa hivyo, ambaye alikuwa Muislamu na akaritadi, kanuni msingi ni kwamba ataadhibiwa kwa uasi wake, na atakayebakia kuwa mshirikina na akawa miongoni mwa wanaoudhuru Uislamu na Waislamu ataadhibiwa kwa kifo au atasamehewa, kwa mujibu wa Imam (kiongozi) wa Waislamu anavyoona inafaa, kama ilivyoelezwa hapo juu katika kifungu hicho. Lakini katika hali zote mbili, Hadith: "Uislamu unafuta yaliyokuwa kabla yake" haiwahusu, kwa sababu tunachojua ni kwamba Hadith: إن الإسلام يجب ما قبله **"Hakika Uislamu Hufuta Yale Yalikuwa Kabla Yake"** inawahusu wale ambao wamesilimu karibuni. Sasa kwa nini Hadith hii inanukuliwa kama dalili katika kifungu hiki, ikijulikana kuwa baadhi ya maswahaba walitumia upanga na kuwauwa Waislamu, kama vile Khalid bin Al-Walid? Na Wahshi bin Harb, Mwenyezi Mungu awe radhi nao, na Mtume (saw) hakuwafanya lolote baada ya kusilimu?

Barak Allah fik, Mwenyezi Mungu aziongoze hatua zako, na akuruzuku ushindi kupitia mikono yake. Salah Fawzi - Al-Quds Al-Sharif

**Jibu:**

Wa Alaikum Assalam Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Inaonekana kuna mkanganyo katika kuelewa suala hilo, kama Hadith ya Mtume (saw) ambayo ilisimuliwa na Ahmad na al-Tabarani kutoka kwa Amr ibn Al-Aas إِنَّ الإِسْلاَمَ يَجُبُّ مَا كَانَ قَبْلَهُ **"Hakika Uislamu Hufuta Yale Yalikuwa Kabla Yake."** Inaashiria kuwa mtu yeyote anayesilimu kutoka kwa makafiri, chochote alichokifanya kabla ya Uislamu kuzingatiwa kama hakikutokea, yaani, hatawajibishwa kwa kile alichofanya kabla ya Uislamu. Kwa hivyo, kuingia katika Uislamu hufuta dhambi ambalo alikuwa amelifanya kabla ya Uislamu kwa sababu Uislamu unafuta kile kilichokuwa kabla yake ... lakini ukweli kwamba Mtume (saw) wakati wa ufunguzi wa

***Endelea... UK 8***

Makka (aliruhusu damu kumwagwa (yaani Kuuwa) ya watu wachache ambao walikuwa wakiudhuru Uislamu na Waislamu katika nyakati za kabla ya Uislamu, damu yao iliruhusiwa kumwagwa (yaani kuuwawa kwao) hata kama wananing'inia mapazia ya Ka'ba), ambayo inaeleweka kwamba watabaki kuwajibika kwa kile walichowadhuru kwacho Waislamu, hata kama wamesilimu, kwa sababu maneno ya Mtume (saw): **(وإن تعلقوا بأستار الكعبة) "Hata kama wananing'inia katika mapazia ya Ka'ba"**. Hii yaashiria kwamba Mtume (saw) hakufanya takhsisi kusilimu kwao, bali aliamuru kuuwawa kwa hali yoyote. Tunafahamu kutokana na hilo kwamba wale wanaoudhuru Uislamu na Waislamu wataadhibiwa kwa yale wanayoyafanya, hata kama watasilimu, hivyo Hadith ya Mtume (saw): إنَّ الإِسْلامَ يَجُبُّ مَا كَانَ قَبْلَهُ **"Hakika Uislamu Hufuta Yale Yalikuwa Kabla Yake."** Haiwajumuishi wao, kwani wako wako nje ya hadith hii, ikimaanisha kuwa madhara yoyote waliyoyasababisha kwa Uislamu na Waislamu, hafutwi na Uislamu, bali watawajibika kwayo, na mambo yao baada ya hapo ni juu ya Imam (kiongozi), akipenda, anawasamehe, na akipenda, anawaadhibu.

Uhalali wa ufahamu huu inaashiriwa kwa yale aliyoyapokea Al-Nasa'i katika Sunan yake kutoka kwa Mus'ab bin Sa'd kutoka kwa babake, aliyesema:

**لَمَّا كَانَ يَوْمُ فَتْحِ مَكَّةَ أَمَّنَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ النَّاسَ إِلَّا أَرْبَعَةَ نَفَرٍ وَامْرَأَتَيْنِ وَقَالَ اقْتُلُوهُمْ وَإِنْ وَجَدْتُمُوهُمْ مُتَعَلِّقِينَ بِأَسْتَارِ الْكَعْبَةِ عِكْرِمَةُ بْنُ أَبِي جَهْلٍ وَعَبْدُ اللَّهِ بْنُ خَطَلٍ وَمَقِيسُ بْنُ صُبَابَةَ وَعَبْدُ اللَّهِ بْنُ سَعْدِ بْنِ أَبِي السَّرْحِ فَأَمَّا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ خَطَلٍ فَأُدْرِكَ وَهُوَ مُتَعَلِّقٌ بِأَسْتَارِ الْكَعْبَةِ فَاسْتَبَقَ إِلَيْهِ سَعِيدُ بْنُ حُرَيْثٍ وَعَمَّارُ بْنُ يَاسِرٍ فَسَبَقَ سَعِيدٌ عَمَّاراً وَكَانَ أَشَبَّ الرَّجُلَيْنِ فَقَتَلَهُ وَأَمَّا مَقِيسُ بْنُ صُبَابَةَ فَأَدْرَكَهُ النَّاسُ فِي السُّوقِ فَقَتَلُوهُ وَأَمَّا عِكْرِمَةُ فَرَكِبَ الْبَحْرَ فَأَصَابَتْهُمْ عَاصِفٌ فَقَالَ أَصْحَابُ السَّفِينَةِ أَخْلِصُوا فَإِنَّ آلِهَتَكُمْ لَا تُغْنِي عَنْكُمْ شَيْئاً هَاهُنَا فَقَالَ عِكْرِمَةُ وَاللَّهِ لَئِنْ لَمْ يُنَجِّنِي مِنْ الْبَحْرِ إِلَّا الْإِخْلَاصُ لَا يُنَجِّينِي فِي الْبَرِّ غَيْرُهُ اللَّهُمَّ إِنَّ لَكَ عَلَيَّ عَهْداً إِنْ أَنْتَ عَافَيْتَنِي مِمَّا أَنَا فِيهِ أَنْ آتِيَ مُحَمَّداً ﷺ حَتَّى أَضَعَ يَدِي فِي يَدِهِ فَلَأَجِدَنَّهُ عَفُوّاً كَرِيماً فَجَاءَ فَأَسْلَمَ وَأَمَّا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ سَعْدِ بْنِ أَبِي السَّرْحِ فَإِنَّهُ اخْتَبَأَ عِنْدَ عُثْمَانَ بْنِ عَفَّانَ فَلَمَّا دَعَا رَسُولُ اللَّهِ ﷺ النَّاسَ إِلَى الْبَيْعَةِ جَاءَ بِهِ حَتَّى أَوْقَفَهُ عَلَى النَّبِيِّ ﷺ قَالَ يَا رَسُولَ اللَّهِ بَايِعْ عَبْدَ اللَّهِ قَالَ فَرَفَعَ رَأْسَهُ فَنَظَرَ إِلَيْهِ ثَلَاثاً كُلَّ ذَلِكَ يَأْبَى فَبَايَعَهُ بَعْدَ ثَلَاثٍ ثُمَّ أَقْبَلَ عَلَى أَصْحَابِهِ فَقَالَ أَمَا كَانَ فِيكُمْ رَجُلٌ رَشِيدٌ يَقُومُ إِلَى هَذَا حَيْثُ رَآنِي كَفَفْتُ يَدِي عَنْ بَيْعَتِهِ فَيَقْتُلُهُ فَقَالُوا وَمَا يُدْرِينَا يَا رَسُولَ اللَّهِ مَا فِي نَفْسِكَ هَلَّا أَوْمَأْتَ إِلَيْنَا بِعَيْنِكَ قَالَ إِنَّهُ لَا يَنْبَغِي لِنَبِيٍّ أَنْ يَكُونَ لَهُ خَائِنَةُ أَعْيُنٍ**

**"Siku ya ufunguzi wa Makka, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alitoa msamaha kwa watu, isipokuwa wanaume wanne na wanawake wawili. Akasema: Wauweni, hata mkiwakuta wananing'inia pazia za Ka'aba. (Walikuwa) 'Ikrimah bin Abi Jahl, 'Abdullah bin Khatal, Miqyas bin Subabah na 'Abdullah bin Sa'd bin Abi As-Sarh. Abdullah bin Khatal alinaswa akiwa ananing'inia pazia za Ka'aba. Sa'id bin Huraith na 'Ammar bin Yasir wote wakamkimbilia, lakini Sa'id, ambaye alikuwa mdogo wa hao wawili, alifika hapo mbele ya 'Ammar, na akamuua. Miqyas bin Subabah alikamatwa na watu sokoni, na wakamuua. 'Ikrimah alisafiri baharini, na akashikwa na tufani. Wahudumu wa meli wakasema: 'Muelekeeni Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi, kwani miungu yenu (ya uwongo) haiwezi kukusaidia chochote katika hali hii.' 'Ikrimah akasema: 'Wallahi, kama hakuna kitu kilichokuja kuniokoa baharini isipokuwa ikhlasi kwa Mwenyezi Mungu basi hakuna kitu chengine kitakachoniokoa ardhini. Ewe Mwenyezi Mungu, nakuahidi kwamba ukiniepusha na tatizo hili nitakwenda kwa Muhammad [saw] na kuweka mkono wangu ndani yake, na nina yakini kwamba nitamkuta ni mkarimu na mwenye kusamehe. Basi akaja, akasilimu. 'Abdullah bin Sa'd bin Abi Sarh alijificha kwenye nyumba ya 'Uthman bin Affan, na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alipowaita watu watoe kiapo chao cha utiifu, alimleta na akamsimamisha mbele ya Mwenyezi Mungu. Mtume [saw]. Akasema (Uthman): Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kubali kiapo cha 'Abdullah.' Akainua kichwa chake na kumtazama mara tatu, akikataa utiifu wake kila mara, kisha akakubali utiifu wake baada ya mara tatu. Kisha akawageukia Maswahaba zake na kusema: Je! Wakasema: Hatukuwa tunajua yaliyomo moyoni mwako, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Kwa nini hukutuonyesha ishara kwa macho yako?' Akasema: "Haimfai Mtume kuwa macho yake yakhini."**

Mtume (saw) aliwataka Waislamu wamuue Abdullah bin Abi al-Sarh ingawa alikuwa amekuja kwake kama Muislamu akiomba kutoa kiapo cha utiifu. Hii inaashiria kuwa damu ya watu hawa iliruhusiwa kumwagwa kwa ukamilifu wake, hivyo kuingia kwao katika Uislamu hakuwakinga na hilo, bali suala lao linarudi kwa Imam (kiongozi), na akitaka, anawaadhibu, na akipenda anawasamehe... Hivyo, ukweli kwamba Mtume (saw) hakuwaadhibu wale kutoka kwa makafiri waliosilimu na walikuwa wakiwadhuru Waislamu, kama ilivyo kwa Ikrimah bin Abi Jahl, kwa mfano itajumuishwa chini ya msamaha wa Imam (kiongozi), kama ilivyoelezwa katika kitabu "Taasisi za Dola katika Khilafah": (Na kwa kuwa Mtume (saw) aliwasamehe baadhi yao baadaye, kama vile Mtume alivyomsamehe Ikrimah bin Abi Jahl. Hivyo basi, inajuzu kwa Khalifa kusimamisha kesi dhidi ya watu hawa au kuwasamehe).

Natumai kuwa hili litamaliza mkanganyiko katika kuelewa suala hili.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**